File - Press releases

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO-19 KATIKA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

***Dodoma, 23 Oktoba, 2021***

**Ndugu Wanahabari**

**Mabibi na Mabwana**

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

## A. UTANGULIZI

**Ndugu Wanahabari,** mtakumbuka kuwa mnamo tarehe 10/10/2021, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan alizindua **Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO 19.** Mpango huo wenye thamani ya Dola za Marekani **milioni 567** sawa na **Shilingi Trilioni 1.3** zilizotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa – IMF kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali inayolenga kuleta maendeleo kwa ustawi wa Taifa na kuwezesha mapambano dhidi ya UVIKO–19. Lengo kuu likiwa ni kufufua uchumi kutokana na athari za ugonjwa huo.

**Ndugu Wanahabari,** leo tumekutana hapa kwa lengo la kutoa taarifa kwa umma kuhusu namna ambavyo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itatumia fedha zilizotolewa chini ya **Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO 19.** Katika Mpango huo, Sekta ya Elimu kwa ujumla imetengewa **Shilingi bilioni 368.9** ambapo Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR–TAMISEMI) imepewa **Shilingi bilioni 304** na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetengewa **Shilingi 64,902,000,000.00** kwa ajili ya miradi tunayosimamia.

**Ndugu Wanahabari,** kabla ya kuanza kuelezea mpango wa Wizara, nianze kwa kumpongeza sana **Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa jitihada zake za kutuletea maendeleo na pia kwa namna anavyotuongoza katika mapambano dhidi ya UVIKO-19. Jitihada zake zimetuwezesha kupata rasilimali fedha za kutekeleza afua za kufufua uchumi kutokana na athari za ugonjwa huo.

Kwa upande wa Wizara, Mpango huo utahusisha maeneo yafuatayo:

i. kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ambapo **Shilingi 1,477,000,000.00** zimetengwa;

ii. kuimarisha Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ambapo kiasi cha **Shilingi 57,985,000,000.00** zimetengwa; na

iii. kuimarisha mazingira ya utoaji wa Elimu ya Ualimu ambapo kiasi cha **Shilingi 5,440,000,000.00** zimetengwa.

**Ndugu Wanahabari,** Athari za UVIKO-19 katika Sekta ya Elimu zilichangiwa na changamoto zilizopo katika mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji, uwiano wa miundombinu kwa wanafunzi na walimu; na uchache wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika taasisi za elimu. Kutokana na changamoto hizo, namshukuru tena **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuipa kipaumbele Sekta ya Elimu katika kutatua changamoto hizo.

## B. UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO-19 KUPITIA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

### 1. Kuimarisha Ujifunzaji na Ufundishaji kwa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalum.

**Ndugu Wanahabari,** katika kuongeza upatikanaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, Serikali imepanga kutumia **shilingi 1,477,000,000.00** kwa ajili ya kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Lengo ni kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi wa Kitanzania anapata elimu bora. Katika kutekeleza hili, fedha hizi zimeelekezwa kufanya mambo yafuatayo:

a) Serikali imepanga kuchapisha vitabu kwa ajili ya wanafunzi 353 wasioona na wenye uoni hafifu 3,591 wa elimu ya sekondari ambapo kiasi cha **Shilingi 707,000,000.00** kimetengwa. Uchapaji wa vitabu hivyo utawezesha uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja na hivyo kumaliza kabisa changamoto ya upungufu wa vitabu kwa wanafunzi hao wa elimu ya sekondari. Vitabu vitakavyochapishwa vitajumuisha:

- nakala **93,366** za vitabu vya kiada vya maandishi yaliyokuzwa (large prints) kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu katika shule za sekondari. **Jedwali Na. 1a**; na
- vitabu vya kiada vya Nukta Nundu (Braile Books) nakala **9,178** kwa ajili ya wanafunzi wasioona wa shule za sekondari. **Jedwali Na. 1b**.

b) Serikali itawezesha ununuzi wa vifaa saidizi kwa wanafunzi 410 wenye mahitaji maalum walioko katika Vyuo Vikuu 11 vya Serikali ambapo kiasi

cha **Shilingi 770,000,000.00** kimetengwa. **Jedwali Na. 1c** linaonesha mchanganuo huo. Aidha, vigezo vilivyotumika kugawa fedha ya Mradi wa IMF kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu wenye mahitaji maalum ni: idadi ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika vyuo husika; na aina ya ulemavu.

## 2. Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ufundi Stadi na Kuongeza Fursa za Upatikanaji Wake

**Ndugu Wanahabari,** katika kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ufundi na Ufundi Stadi na kuongeza fursa za upatikanaji wake, Serikali imepanga kutumia **Shilingi 57,985,000,000.00** ambazo zitawezesha kutekeleza yafuatayo:

a) kukamilisha ujenzi na kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo **25** vya Ufundi Stadi vya Wilaya ambapo kiasi cha **Shilingi 28,762,344,780.75** kimetengwa. Ukamilishaji wa Vyuo hivi utawezesha ongezeko la takribani **wanafunzi 30,000** katika Vyuo vya VETA. Orodha ya Vyuo hivyo na gharama itakayotumika inaoneshwa katika **Jedwali Na. 2.**

b) Serikali imepanga kukamilisha ujenzi na kuweka samani katika Vyuo vya VETA vinne (4) vya ngazi ya Mkoa katika mikoa ya Njombe, Rukwa, Simiyu na Geita ambapo **Shilingi 18,706,339,249.00** zimetengwa. Kukamilika kwa vyuo hivi kutaongeza jumla ya nafasi za **wanafunzi 5,600** katika mafunzo ya ufundi stadi. Mchanganuo wa gharama kwa kila Chuo unaoneshwa katika **Jedwali Na. 3a.**

Aidha, Serikali imepanga kutumia **Shilingi 1,046,557,536.08** kujenga mabweni katika Chuo cha Ualimu wa Ufundi Morogoro (MVTCC). Lengo likiwa ni kuongeza fursa za mafunzo ya Ualimu wa ufundi stadi ili kuendana na ongezeko la vyuo vya ufundi stadi nchini. Gharama ya ujenzi zinaoneshwa katika **Jedwali Na. 3c.**

c) Katika kuimarisha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (Folk Development Colleges - **FDCs**), Serikali imepanga kutumia **Shilingi 6,800,000,000.00** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na mitambo ya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo **34.** Mchanganuo wake unaonekana katika **Jedwali Na. 3b.**

**Ndugu Wanahabari,** ikumbukwe kuwa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (Folk Development Colleges – FDCs) vilianzishwa mwaka 1975 kutokana na wazo la **Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere, Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.** Vyuo hivi vilianzishwa kwa falsafa ya kutoa nafasi kwa wananchi kujifunza kupitia mfumo usio rasmi katika mazingira yao ili kuleta maendeleo ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni kwa kuzingatia rasilimali na fursa zilizopo katika maeneo yao.

**Ndugu Wanahabari,** kwa muktadha huo, natumia nafasi hii kwa mara nyingine kumpongeza tena **Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuendelea kumuenzi Baba wa Taifa kwa vitendo. Kitendo cha kuboresha Vyuo hivi

kutawezesha malengo ya kuanzishwa kwake kuendelea kutimizwa ambapo jumla ya **wanachuo 9,804** watanufaika na vifaa vitakavyonunuliwa na hivyo kuimarisha ujuzi watakaoupata.

d) Katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa vitendo katika **Chuo cha Ufundi Arusha (ATC), Shilingi 2,669,758,432.08** zimetengwa kwa lengo la kukamilisha Jengo la Chuo ambalo litakuwa na **kumbi 2 za mihadhara**, **vyumba 6 vya madarasa**, **maabara 7** na **ofisi 26.** Baada ya kukamilika jengo litakuwa na uwezo wa kuhudumia **wanachuo wapatao 911** na **walimu 81** kwa wakati mmoja na hivyo kuongeza fursa ya upatikanaji wa mafunzo ya ufundi katika mazingira bora zaidi. Gharama za ujenzi zimeanishwa katika **Jedwali Na. 3c**.

**Ndugu Wanahabari,** uimarishaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi utawezesha kuandaa rasilimaliwatu kwa maendeleo ya uchumi wa viwanda na kuongeza tija katika uzalishaji mali. Aidha, itachangia katika kupunguza tatizo la ajira kwa vijana na hivyo kutekeleza agenda ya maendeleo na ustawi wa jamii kwa ufanisi.

## 3. Kuimarisha Mazingira ya Utoaji wa Elimu ya Ualimu

**Ndugu Wanahabari,** katika kuimarisha mazingira ya uandaaji wa walimu na kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu ya Ualimu, Serikali katika mpango huu imepanga kujenga vyumba vya **madarasa 41**, **kumbi 3 za mihadhara na mabweni 15** na kuweka samani katika majengo hayo. Ujenzi huo utazingatia mahitaji ya ufundishaji na ujifunzaji, utekelezaji wa afua hizi utagharimu jumla ya **Shilingi 5,440,000,000.00** kwa kutekeleza yafuatayo:

i. kujenga kumbi za mihadhara katika Vyuo vitatu (3) vya Ualimu ambavyo ni Butimba, Kasulu na Morogoro kwa kutumia **Shilingi 1,092,158,767.04**;
ii. kujenga madarasa katika Vyuo vya Ualimu 15 ambapo **Shilingi 1,536,774,915.00** zimetengwa; na
iii. kujenga mabweni katika Vyuo vya Ualimu 15 ambapo **Shilingi 2,811,066,318.00** zimetengwa. **Jedwali Na. 4** limeainisha mchanganuo kwa kila eneo.

**D: HITIMISHO NA MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI**

**Ndugu Wanahabari,** nitumie fursa hii kuhitimisha taarifa kuhusu namna Wizara ilivyojipanga kutekeleza **Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19.** Nawaelekeza watendaji wa Wizara na Taasisi zitakazotekeleza shughuli za Mpango kuzingatia yafuatayo:

i. Ifikapo tarehe 30/10/2021 kukamilisha maandalizi ya utekelezaji wa miradi yote mapema ikiwa ni pamoja na: kuandaa mpango kazi utakaoainisha hatua mabalimbali za taratibu za manunuzi ya huduma na vifaa na lini ununuzi utafanyika hadi kukamilika kwa mradi;
ii. Ununuzi wa vifaa vyote ufanyike kwa kuzingatia bei ya soko;
iii. Utekelezaji wa miradi hii ukamilike kabla au ifikapo tarehe 30 Mei 2022;
iv. Matokeo ya utekelezaji wa miradi yaendane na thamani ya fedha zilizotolewa;

v. Katibu Mkuu aandae mfumo wa uratibu, usimamizi na ufuatiliaji wa Mradi utakaowezesha kubaini changamoto zitakazokuwa zinajitokeza na kuchukua hatua stahiki kwa wakati; na

vi. Taarifa za utekelezaji zitolewe kila mwezi kwa Katibu Mkuu.

**Angalizo muhimu ni kwamba Fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19 hazihusishi posho ya aina yoyote. Hivyo, narudia tena kusisitiza maelekezo ya Mheshimiwa Rais kuwa, fedha hizi zisitumike kulipia posho ya aina yoyote na viongozi wote wa Taasisi zinazonufaika. Nitafuatilia kwa karibu kuhakikisha maagizo ya Mheshimiwa Rais kuhusu matumizi sahihi ya fedha hizi yanatekelezwa kikamilifu.** Nawapa tahadhari watumishi wote wa Wizara wanaohusika na utekelezaji wa Mpango huu kuwa nitakuwa makini katika kuhakikisha kuwa mpango huu unatekelezwa kwa ufanisi kuanzia hatua ya maandalizi hadi utakapokamilika kwa wakati uliopangwa.

Ahsanteni kwa Kunisikiliza

***"Tunaboresha Elimu yetu, Kazi iendelee"***

Mhe. Prof. Joyce L. Ndalichako (Mb.)

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**